**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

**RISALA YA MWENYEKITI WA TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI MHE. JAJI (RUFAA) JACOBS C. M. MWAMBEGELE KUHUSU ZOEZI LA KUPIGA KURA KWENYE UCHAGUZI MDOGO WA UBUNGE KATIKA JIMBO LA ISMANI NA MADIWANI KATIKA KATA 12 ZA TANZANIA BARA UTAKAOFANYIKA**

**TAREHE 01 JUNI, 2026**

***Ndugu Wananchi;***

Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 49(1)(b), (2) na (4), 57(2) na 68(2) vya Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, Sura ya 343, kesho tarehe 01 Juni, 2026 kutakuwa na uchaguzi mdogo wa ubunge katika Jimbo la Ismani Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, Mkoa wa Iringa na Madiwani katika kata 12 za Tanzania Bara.

Kata hizo ni Mzimuni iliyopo Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni; Zongomera, Halmashauri ya Manispaa ya Kahama; Itilo, Halmashauri ya Mji Nzega; Ketare, Halmashauri ya Mji Tarime na Nyumbigwa, Halmashauri ya Mji Kasulu.

Nyingine ni Kata ya Kala iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi; Ziba, Halmashauri ya Wilaya Igunga; Kamsisi, Halmashauri ya Wilaya ya Mlele; Nyamugali, Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe; Namasakata Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru; Bwongera, Halmashauri ya Wilaya ya Chato na Kibiti, Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti.

*Ndugu Wananchi;*

Katika Uchaguzi huu, jumla ya wagombea **108** kutoka katika vyama vya siasa **17** wanawania nafasi wazi ya ubunge na udiwani katika maeneo niliyoyataja.

Jimbo la Ismani lina wagombea 17 wa nafasi ya Ubunge ambapo kati ya wagombea hao wagombea nane (08) sawa na asilimia 47.06 ni wanaume na wagombea tisa (09) sawa na asilimia 52.94 ni wanawake. Kata 12 zinazofanya uchaguzi mdogo wa udiwani zina jumla ya wagombea 91 ambapo kati ya hao wagombea 61 sawa na asilimia 67.03 ni wanaume na wagombea 30 sawa na asilimia 32.97 ni wanawake. Kwa namna ya pekee, Tume inavipongeza vyama vilivyoshiriki na wagombea waliojitokeza kushiriki.

Aidha, jumla ya Wapiga Kura **222,218** walioandikishwa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura watashiriki kwenye uchaguzi huo ambapo wapiga kura **89,753** wapo kwenye Jimbo la Ismani na wapiga kura **132,465** wapo kwenye kata 12 zitakazofanya uchaguzi mdogo.

Aidha, jumla ya vituo **628** vya kupigia kura vitatumika ambapo vituo **277** vipo kwenye Jimbo la Ismani na vituo **351** vipo kwenye kata **12** zitakazofanya uchaguzi mdogo.

***Ndugu wananchi,***

Natumia fursa hii kuvikumbusha Vyama vya Siasa vinavyoshiriki uchaguzi huo mdogo utakaofanyika kesho tarehe 01 Juni, 2026 kuzingatia wajibu wao wa kuweka mawakala katika vituo vyote vya kupiga, kuhesabu na kujumlishia kura. Wasimamizi wa uchaguzi katika jimbo na kata husika, wamekamilisha taratibu zinazoweka mazingira yanayowawezesha mawakala wa vyama vya siasa kufuatilia mchakato mzima wa uchaguzi.

Mawakala hao, wanawajibika kuwakilisha na kulinda maslahi ya vyama na wagombea wao. Hivyo, wanapaswa kuzingatia Sheria, Kanuni, taratibu za Uchaguzi na maelekezo ya Tume katika utekelezaji wa majukumu yao vituoni.

*Ndugu Wananchi;*

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inavikumbusha vyama vya siasa, wagombea, mawakala, wapiga kura na wananchi wote kwa ujumla kuzingatia mambo yafuatayo: -

i. Mpiga Kura, anatakiwa kwenda katika kituo alichojiandikisha na kadi yake ya mpiga kura siku ya uchaguzi.

ii. Wapiga Kura watakaoruhusiwa kupiga kura ni wale walioandikishwa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

iii. Mpiga kura awapo kituoni anatakiwa kutoa kipaumbele kwa wapiga kura wenye mahitaji maalumu kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga watakaokuwa nao kituoni.

iv. Watu wenye mahitaji maalumu wanaruhusiwa kwenda kituoni na wasaidizi wao.

v. Vituo vitafunguliwa saa 01:00 asubuhi na kufungwa saa 10:00 jioni. Ifikapo muda wa kufunga kituo saa 10:00 kamili jioni, kama wapiga kura bado wapo kwenye mistari, mlinzi wa kituo atasimama nyuma ya mtu wa mwisho na zoezi la upigaji kura litaendelea hadi wapiga kura waliopo kwenye mstari watakapomalizika. Mpiga kura atakayefika zaidi ya muda wa kufunga kituo hataruhusiwa kupiga kura.

vi. Baada ya kumaliza kupiga kura, mpiga kura anatakiwa kuondoka eneo la kituo cha kupigia kura; na

vii. Mpiga kura awapo kituoni, anatakiwa kufuata maelekezo yote atakayopewa na karani mwongozaji wapiga kura.

*Ndugu Wananchi;*

Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 4, 14(2), 19(3), 84(3)(a) na (b) na 164 vya Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, Sura ya 343, vikisomwa pamoja na kifungu cha 26 cha Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 292, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, ilitoa maelekezo ya kisera katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 kwa wapiga kura kama ifuatavyo:

i. Kwa mpiga kura asiye na picha katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura lakini ana kadi ya Mpiga Kura yenye taarifa binafsi zilizomo katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, **ARUHUSIWE KUPIGA KURA;**

ii. Kwa mpiga kura ambaye ana kadi yenye namba ya mpiga kura inayotofautiana na namba ya mpiga kura iliyomo katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura lakini taarifa nyingine zote ikiwemo picha na majina yaliyopo katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ni sawa kama ilivyo katika kadi ya mpiga kura aliyonayo; **ARUHUSIWE KUPIGA KURA;**

iii. Kwa mpiga kura ambaye ameandikishwa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na taarifa zake zipo katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura lililopo katika kituo husika, lakini amepoteza kadi yake au kadi yake imeharibika, **ARUHUSIWE KUPIGA KURA** kwa kutumia mojawapo ya vitambulisho vituatavyo:

   a) Kitambulisho cha Taifa (NIDA);

   b) Leseni ya udereva; au

   c) Pasi ya kusafiria (Passport)

Lakini kwa sharti kwamba, majina yake yaliyopo katika kitambulisho atakachowasilisha mpiga kura, ni lazima yafanane na majina yote kama yalivyo katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

iv. Kwa mpiga kura ambaye ana kadi ya kupigia kura lakini taarifa zake hazipo katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura **ASIRUHUSIWE KUPIGA KURA.**

Nawakumbusha nyote, kuzingatia maelekezo haya ya kisera.

***Ndugu wananchi;***

Mwisho lakini siyo kwa umuhimu, Tume inatoa rai kwa wapiga kura kwenye maeneo yenye uchaguzi, kujitokeza kwa wingi kwenye vituo vya kupigia kura hapo kesho, ili kuwachagua viongozi wanaowataka.

Imetolewa leo tarehe 31 Mei, 2026; na

Jaji (Rufaa) Jacobs C.M. Mwambegele

**MWENYEKITI**

**<u>TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI</u>**